# SERIKALI MTANDAO

Tuijenge Serikali kidijtali

ISO 9001: 2015 CERTIFIED

www.ega.go.tz

Toleo la 13 | Julai - Septemba 2025

# e-Mrejesho V2 Kinara wa Tuzo ya WSIS 2025




Bodi ya kwanza ya wakurugenzi ya e-GA yaacha Historia >>>Uk 07

Mageuzi ya TEHAMA yaimarisha Sekta ya Ushirika. >>>Uk 09

Mgongo Wako,Afya yako Tambua Hatari, Epuka Maumivu >>>Uk 18

Vijana na TEHAMA >>>Uk 22

# YALIYOMO

NUKUU
Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya e-GA 3

TAHARIRI
GOVESB: Muhimili wa Mawasiliano ya Kidijitali Serikalini 4

DIRA YETU
Serikali Mtandao kupitia Viwango na Miongozo 5

HABARI
e-Mrejesho V2 Kinara wa Tuzo ya WSIS 2025 6

HABARI
Bodi ya wakurugenzi ya kwanza yaacha historia 7

MAKALA
Mageuzi ya TEHAMA yaimarisha Sekta ya Ushirika Tanzania 9

HABARI
Ushirikiano wa e-GA na Sekta ya Kilimo wazidi kuimarika 10

HABARI
Tovuti yatajwa kuwa nyenzo muhimu ya Taarifa za Serikali 12

HABARI
Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA yameimarisha wazi na Ufanisi Serikalini 13

HABARI
Programu ya Mafunzo kwa Vitendo 2025 yazinduliwa Dodoma 14

VIJANA NA TEHAMA
Tembea Kidijitali : Mageuzi ya Huduma za Umma Kupitia e-Tour 16

AFYA
Mgongo Wako, Afya Yako: Tambua Hatari, Epuka Maumivu 18

WASEMAVYO WADAU
Mafunzo kwa Vitendo 22

Matukio katika Picha 23

Kumbukumbu 25

# MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI YA e-GA



Serikali Mtandao ni chombo muhimu cha kuleta mageuzi ya kiutendaji ndani ya serikali; inaleta uwazi, uwajibikaji, ufanisi, na upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi. Mamlaka ya Serikali Mtandao inadhamiria kutekeleza mabadiliko haya kwa kuhakikisha mifumo ya TEHAMA inasimamiwa kwa weledi, inatumika kwa tija, na inalinda usalama wa taarifa. Kwa kushirikiana na taasisi zote za umma, tunalenga kujenga serikali ya kisasa inayojibu mahitaji ya wananchi kwa haraka, kwa usahihi, na kwa uwazi.

**Dkt. Mussa Kissaka**
**Mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi**

# GOVESB

## Muhimili wa Mawasiliano ya Kidijitali Serikalini




**Bi. Subira Kaswaga**
**Meneja Mawasiliano**

Katika zama hizi za mageuzi ya kidijitali, Serikali yoyote inayotamani kutoa huduma bora, za haraka na zenye ufanisi kwa wananchi wake, haiwezi kufanikisha hilo bila kuwa na mifumo inayowasiliana na kubadilishana taarifa kwa ufanisi. Hapa ndipo mfumo wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini yaani **'Government Enterprise Service Bus – GOVESB'** unapochukua nafasi ya kipekee kama muhimili wa mawasiliano ya mifumo ya TEHAMA ndani ya serikali.

Mfumo wa **GOVESB** ni jukwaa la kati linalowezesha mifumo mbalimbali ya serikali kuwasiliana, kubadilishana taarifa kwa usalama, haraka na kwa viwango vilivyokubaliwa, bila kujali tofauti za kiteknolojia kati ya mifumo hiyo. Hii ni hatua muhimu katika kuhakikisha uwepo wa "Serikali Moja ya Kidijitali, dhana ambayo imeendelea kuwa dira ya utekelezaji wa Serikali Mtandao kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA).

Ujenzi wa Mfumo huu unatokana na agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na kifungu cha 48 (1) cha Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019, inayoielekeza e-GA kutengeneza Mfumo utakaowezesha ubadilishanaji wa taarifa Serikalini kupitia TEHAMA.

Kupitia mfumo wa GOVESB, taasisi za umma sasa zinaweza kuunganisha huduma zao kwa njia shirikishi, na hivyo kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Badala ya mwananchi kuhangaika kutoka ofisi moja hadi nyingine kufuatilia taarifa zinazohusu huduma mbalimbali, sasa taasisi zenye mifumo iliyounganishwa zinaweza kupokea, kuthibitisha na kushughulikia taarifa moja kwa moja kwa wakati kupitia mfumo huu.

Kwa sasa, zaidi ya taasisi **140** za umma zimeunganishwa na mfumo wa **GOVESB** zikiwemo Wizara, Wakala, Mamlaka, Idara zinazojitegemea na Mashirika ya Umma. Pia, zaidi ya mifumo **200** inawasiliana na kubadilishana taarifa ikiwemo;

Mfumo wa vitambulisho wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), umeunganishwa na mifumo ya taasisi mbalimbali za Serikali kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Usajili wa Vizazi na Vifo (RITA), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) n.k.

Aidha, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imeendelea kusimamia na kuboresha mfumo wa **GOVESB** ili kuhakikisha kuwa miundombinu na usalama wa taarifa inaimarika kwa kuzingatia viwango vya kitaifa vya ubadilishanaji wa data. Kupitia uwekezaji huu, Serikali inaimarisha udhibiti wa mapato, uwajibikaji na ushirikishwaji wa wananchi.

Hata hivyo, mafanikio ya mfumo huu hayawezi kupatikana bila ushirikiano wa karibu kati ya taasisi za umma. Nitoe rai kwa taasisi zote za Serikali kutambua umuhimu wa **GOVESB** na kuhakikisha kuwa mifumo yao inaunganishwa. Hili si suala la kiufundi tu, bali ni la kimkakati kwa mustakabali wa utoaji wa huduma za umma kwa njia ya kidijitali

Kwa pamoja, tuendelee kuijenga Serikali Mtandao ya kisasa yenye mifumo inayoongea, inayoshirikiana, na inayolenga mahitaji ya wananchi.


## BODI YA UHARIRI

| | |
|---|---|
| Mwenyekiti | Eng. Benedict B. Ndomba<br>Mkurugenzi Mkuu |
| Mhariri | Subira J. Kaswaga<br>Meneja Mawasiliano |
| Wajumbe | Erick Kalembo<br>Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshaji<br>SACP. Hamis Ali<br>Mkaguzi mkuu wa Ndani<br>SACP. Rafael Ruthahiwa<br>Meneja wa Huduma za Sheria<br>Long'ida Oltetiai<br>Meneja wa Huduma kwa wateja na Takwimu |



Mhandisi Benedict Ndomba
Mkurugenzi Mkuu e-GA

# Kujenga Msingi Imara wa Serikali Mtandao kupitia Viwango na Miongozo

Sheria ya Serikali Mtandao **Na. 10 ya Mwaka 2019**, imeipa jukumu Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kuandaa na kusimamia Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, ili kujenga Serikali Mtandao yenye kukidhi mahitaji na kuleta tija iliyokusudiwa kwa taifa.

Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, huelekeza taratibu za kuzingatia, pamoja na vigezo katika ujenzi na

usimamizi wa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA Serikalini, ili kuhakikisha inakuwa na thamani halisi lakini pia kuondoa urudufu wa mifumo.

Kwa muktadha huo, e-GA imeendelea kutekeleza wajibu wake kwa kutoa miongozo na viwango mbalimbali vinavyohusu usanifu na usimamizi wa mifumo na miundombinu ya serikali mtandao. Kwa kueleza taratibu zinazopaswa kufuatwa na taasisi za umma kabla ya kuanzisha miradi ya TEHAMA Serikalini.

Umuhimu wa Kuzingatia Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao.

**1.Kuhakikisha Mifumo inayojengwa inawasiliana:** Viwango vya Serikali Mtandao vinasaidia mifumo ya taasisi mbalimbali ya Serikali kuwasiliana na kubadilishana taarifa ikiwa itahitajika kufanya hivyo, bila ya kuwa na vikwazo vya kiteknolojia.

**2.Kulinda Usalama wa Taarifa za Serikali:** Miongozo ya usalama wa TEHAMA inalinda taarifa za Serikali dhidi ya matishio ya kimtandao ya ndani na nje.


**3.Kupunguza Gharama:** Kwa kuzingatia viwango na miongozo, taasisi huepuka

urudufu wa mifumo Serikalini na kuwezesha kuwa na mifumo michache inayokidhi mahitaji ya taasisi na Serikali kwa ujumla.

Uandaaji wa miongozo na viwango vya Serikali Mtandao hufanywa na Mamlaka kwa ushirikiano na taasisi mbalimbali za umma, ili kuhakikisha inakidhi matarajio ya Serikali. Aidha, Mamlaka itaendelea kuboresha viwango na miongozo ya Serikali Mtandao kadiri itakavyohitajika kutokana na mabadiliko ya teknolojia.

Nazikumbusha taasisi za Umma kuhakikisha zinazingatia Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika ujenzi na usimamizi wa miradi ya TEHAMA, ili kuwa na miradi sahihi yenye kuleta tija kwa Taifa.

Ikumbukwe kuwa, uzingatiaji wa viwango na miongozo ya Serikali Mtandao, huongeza uwajibikaji na ujenzi wa Serikali imara ya kidijitali.



# e-Mrejesho V2 Kinara wa Tuzo ya WSIS 2025



*Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Jerry William Silaa (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na watumishi Wizara pamoja na e-GA mara baada ya kukabidhiwa tuzo za WSIS 2025 Jijini Geneva USWIS*

Na. Catherine Peter | Afisa Habari Mwandamizi

Tanzania kupitia Mfumo wa e-Mrejesho Toleo la pili (e-MrejeshoV2) imeibuka mshindi katika kipengele cha Serikali Mtandao, kwenye Tuzo za Mkutano wa Dunia wa Jumuiya ya TEHAMA Mwaka 2025 (World Summit on the Information Society -WSIS 2025).

Utoaji wa tuzo za WSIS umefanyika Julai 7 Mwaka 2025 katika mkutano wa Tukio la Ngazi ya Juu la Jukwaa la WSIS+20 (WSIS+20 Forum High-Level Event), uliofanyika mjini Geneva USWIS kuanzia tarehe 7 hadi 11 Julai Mwaka 2025. Mhe. Jerry Silaa (Mb) Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari alipokea tuzo hiyo kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Tuzo hizo ambazo huratibiwa na Shirika la Mawasiliano la Umoja wa Mataifa (International Telecommunications Union – ITU) zinalenga kutambua na kuchochea miradi bunifu, inayotumia TEHAMA katika kuchangia maendeleo endelevu duniani.

Akieleza kuhusu ushindi huo, Meneja Mawasiliano wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bi. Subira Kaswaga amesema, Mfumo wa e-Mrejesho toleo la pili (V2), umeibuka mshindi wa tuzo hiyo katika kipengele cha Serikali Mtandao (e-Government AL C7), kati ya mifumo **360** ya TEHAMA iliyofuzu hatua ya awali ya mchujo kutoka kwa zaidi ya maombi 1000 ya mifumo ya kidijitali yaliyowasilishwa kutoka mataifa mbalimbali duniani.

Baada ya mchujo wa awali, mfumo wa eMrejesho ulifanikiwa kuingia kundi la tano bora kupitia taarifa iliyopokelewa na e-GA kutoka ITU kwa njia ya baruapepe. Hii ilikuwa ni hatua muhimu kwa e-GA na kudhihirisha namna Watanzania walivyoshiriki kupiga kura, na kuwezesha mfumo huo kuingia katika tano bora.

"Nifuraha kubwa kuona wananchi wameweza kuitikia wito na kuwa wazalendo kwa kufanya kazi kubwa ya kuhakikisha wanapiga kura kwa wingi na hatimaye tuzo imekuja nyumbani, kwa niaba ya e-GA tunawashukuru sana" amesema Bi. Subira.

Mfumo wa e-Mrejesho (V2) umesanifiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), ukiwa umeboreshwa kwa kutumia teknolojia ya Akili Unde (Artificial Intelligence - AI) katika kukusanya maoni ya wananchi. Mfumo huu unasimamiwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mfumo wa eMrejesho unapatikana kwa njia tatu ambazo ni kupitia simu ya mkononi kwa kubofya *152*00# na kisha kuchagua namba 8 na kisha namba 2 na kisha kufuata maelekezo. Pia, kupitia simu janja kwa kupakua Aplikesheni tumizi (Mobile App) ya e-Mrejesho inayopatikana kwenye 'Play Store na Apps Store', na kwa njia ya Tovuti ya https://e-mrejesho.gov.go.tz

# Bodi ya Kwanza ya Wakurugenzi e-GA yaacha alama ya Kihistoria

## Miaka Mitatu ya Mafanikio

- Ushindi wa Tuzo Kimataifa
- Uimarishaji na Usalama wa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA Serikalini.



*Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya e-GA, Dkt. Mussa Kissaka akiongoza kikao cha mwisho cha Bodi hiyo kilichofanyika katika Ofisi za e-GA zilizopo Iringa*

Na Subira Kaswaga | Meneja Mawasiliano

Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imehitimisha rasmi muda wake wa uongozi wa miaka mitatu tangu kuanzishwa kwake Oktoba 2022, ikiwa ni Bodi ya kwanza kuiongoza taasisi hiyo muhimu katika mageuzi ya kidijitali Serikalini.

Akizungumza hivi karibuni Mkoani Iringa, Mwenyekiti wa Bodi hiyo Dkt. Mussa Kissaka, alieleza kwa fahari mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha uongozi wake, akisisitiza kuwa mafanikio hayo ni matokeo ya mshikamano mzuri uliopo kati ya Bodi na Menejimenti ya e-GA.

"Tukiwa kama Bodi ya kwanza ya e-GA, tumefanikisha kusimamia kikamilifu utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka, huku tukihakikisha mustakabali bora wa taasisi na watumishi wake," alisema Dkt. Kissaka.

Mafanikio Makubwa Yaliyopatikana

### 1.Tuzo za Kimataifa

- Mfumo wa e-Mrejesho V2 ulishinda tuzo ya World Summit on the Information Society (WSIS) 2025 kwenye kipengele cha Serikali Mtandao.
- Mwaka 2024, mfumo wa e-Mrejesho ulitunukiwa Tuzo ya Umoja wa Mataifa ya Ubunifu katika Huduma za Umma (UN Public Service Innovation Award) kwa kutambuliwa kama jukwaa la kidijitali la kupokea na kufanyia kazi maoni na malalamiko ya wananchi.
- Kwa mujibu wa ripoti ya GovTech Maturity Index 2022 ya Benki ya Dunia, Tanzania ilipanda daraja kutoka nafasi ya 90 hadi ya 26 duniani,

na kushika nafasi ya pili barani Afrika, nyuma ya Mauritius pekee, katika ukomavu wa matumizi ya TEHAMA Serikalini.

## 2.Uimarishaji wa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA Pamoja na Usalama wa Serikali Mtandao.

- Bodi iliongoza kwa mafanikio juhudi za kuimarisha usimamizi na udhibiti wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA serikalini, hali iliyopelekea huduma za Serikali Mtandao kuwa thabiti na salama zaidi. Hii inaenda sambamba na ujenzi wa Mfumo wa Uthibitisho wa Njia ya Pili 'Multifactor Authentication', wa NGAO, ambao unalenga kuimarisha usalama wa taarifa za Serikali zilizopo katika mifumo na muindombinu ya TEHAMA.
- Utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuhusu mawasiliano ya mifumo ya Serikali kupitia Mfumo Mkuu wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini – GoVESB umefanikiwa kwa kiwango kikubwa. Hadi sasa Mifumo ya TEHAMA zaidi ya 200 imeunganishwa na inabadilishana taarifa kupitia mfumo huu.


Aidha, Mjumbe wa Bodi, Prof. Aloyce Mvuma alisisitiza umuhimu wa Menejimenti ya e-GA kuendeleza kazi nzuri iliyoasisiwa na Bodi hiyo, hasa kuhakikisha taasisi za umma zinaunganishwa kikamilifu kwenye mfumo wa GoVESB. Aidha, aliishauri e-GA kuanza mapema utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050, kwa kuainisha maeneo ya vipaumbele vya Serikali Mtandao.

Akizungumza kwa niaba ya Menejimenti, Meneja wa Huduma za Sheria e-GA, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi (SACP) Rafael Rutaihwa, aliishukuru Bodi kwa uongozi wake madhubuti na mchango mkubwa katika kujenga misingi imara ya taasisi.

Uongozi wa Bodi ya kwanza ya e-GA umeacha alama isiyofutika katika historia ya taasisi na maendeleo ya TEHAMA Serikalini kwa ujumla. Kupitia mafanikio haya, Tanzania imejidhihirisha kuwa kinara katika matumizi ya teknolojia kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa wananchi na kujenga msingi imara wa serikali ya kidijitali.



> **"Tutahakikisha tunayaenzi na kuyaendeleza yote mema mliyoyaacha, huku tukidumisha nidhamu, weledi na uwajibikaji katika kutekeleza majukumu ya Serikali Mtandao."**
>
> SACP. Rafael Rutaihwa
>
> **SACP. Rafael Rutaihwa**




# Mageuzi ya TEHAMA yaimarisha Sekta ya Ushirika Tanzania

**Mfumo wa MUVU waleta uwazi, uwajibikaji na udhibiti wa mapato**

Na. Benchine Bago | Afisa Habari

Kwa muda mrefu ushirika umekuwa ni moja ya taasisi muhimu zinazochangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi, hasa katika maeneo ya vijijini. Ushirika unatoa fursa kwa wanachama wake kushirikiana kwa pamoja katika uzalishaji, masoko, na upatikanaji wa huduma mbalimbali za kifedha na kijamii.

Hata hivyo, licha ya umuhimu huo, changamoto mbalimbali zikiwemo kutokuwepo kwa usimamizi makini, upotevu wa kumbukumbu, pamoja na ukosefu wa uwazi zimekuwa zikikwamisha ufanisi wa vyama vingi vya ushirika. Hali hii ilizorotesha ustawi wa vyama vya ushirika.

Katika kukabiliana na changamoto hizi, Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU), ulianzishwa kama suluhisho la kiteknolojia linalolenga kuboresha usimamizi na utendaji wa vyama vya ushirika.

MUVU ni mfumo wa kidijitali unaorahisisha ukusanyaji, uhifadhi, uchambuzi na utoaji wa taarifa muhimu zinazohusu uendeshaji wa ushirika. Kupitia mfumo huu, ushirika unaweza kufuatilia kwa ufanisi michango ya wanachama, mapato, matumizi, pamoja na kutoa taarifa kwa uwazi zaidi kwa wanachama na wadau wengine.

Mfumo wa MUVU umesanifiwa, umejengwa na unaendeshwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC). Makala hii inachambua jinsi mfumo wa MUVU ulivyoleta mabadiliko katika uendeshaji wa ushirika na mafanikio yaliyopatikana ili kufahamu nafasi ya teknolojia katika kuboresha ufanisi, uwazi na uwajibikaji ndani ya vyama vya ushirika.

Mrajisi na Mtendaji Mkuu wa TCDC Dkt. Benson Ndiege amebainisha kwamba mfumo wa MUVU umerahisisha utendaji kazi wa vyama vya ushirika takribani 6000, ikiwa ni pamoja na usimamizi na uendeshaji wa vyama hivyo kwa kuwa kila kitu sasa kinafanyika kidijitali.

## Kuondoa Urasimu, Rushwa na Ubadhilifu

Kupitia mfumo wa MUVU, urasimu na mianya ya rushwa katika usimamizi wa vyama vya ushirika nchini umepungua kwa kiwango kikubwa, na sasa changamoto hizi zinaendelea kuwa historia katika safari ya maendeleo ya ushirika. Hatua hii imeongeza kwa kiasi kikubwa imani ya wanachama kwa viongozi wao, kwani maamuzi yanatolewa kwa uwazi na kwa wakati.

"Kwa sasa, kupitia mfumo huu wa MUVU, mwanachama aliyepo Kigoma, Tabora au Mtwara anaweza kuwasilisha bajeti au kuomba usajili wa chama kipya kwa njia ya kidijitali

bila kulazimika kusafiri. Maombi yanachakatwa na kupitishwa au kukataliwa kwa haraka kwa kuzingatia vigezo stahiki, bila hitaji la kukutana ana kwa ana na mtendaji," amebainisha Dkt. Ndiege.

Mfumo wa MUVU pia umeimarisha ufuatiliaji wa rasilimali za ushirika, hatua ambayo imewezesha udhibiti thabiti wa mali na matumizi yake. Kwa kuwa taarifa zote za kifedha na kihuduma zinaonekana kwa uwazi ndani ya mfumo, nafasi ya ubadhirifu au matumizi mabaya ya mali za ushirika imepungua kwa kiasi kikubwa. Jitihada hizi zimesaidia kupunguza migogoro ya mara kwa mara ndani ya vyama.

Uthibitishaji wa Vyama Hai na Uimarishaji wa Takwimu Kupitia Mfumo wa MUVU

Miaka kadhaa kabla ya kuanzishwa kwa mfumo wa MUVU, nyaraka mbalimbali zilionyesha kuwa Tanzania ilikuwa na zaidi ya vyama vya ushirika 12,000. Hata hivyo, uchambuzi wa kina ulibaini kuwa idadi hiyo haikuwa sahihi, kwani baadhi ya vyama vilikuwa vimeshakufa na kusitisha shughuli zake, huku vingine vikiwa ni vyama hewa, ambavyo havikuwa na uhalisia wala uhalali wa kisheria.

Usajili wa vyama hivi kupitia mfumo wa MUVU uliwezesha kufanya uhakiki wa kina na kuondoa taarifa potofu, hivyo kubainisha vyama ambavyo viko hai na vinavyotekeleza majukumu yake ipasavyo. Kupitia hatua hii, sekta ya ushirika imepata uthabiti zaidi kutokana na kupatikana kwa takwimu



**Dkt. Benson Ndiege**
Mtendaji Mkuu wa TCDC

sahihi kuhusu makusanyo, idadi halisi ya vyama, pamoja na hali ya utendaji kazi wa kila siku.

Mfumo wa MUVU umesaidia pia kupanga na kutekeleza bajeti kwa ufanisi zaidi, kwa kuwa mipango sasa inafanyika kwa kuzingatia takwimu halisi badala ya makadirio yasiyo na uhakika.

"Mfumo huu umepunguza muda na gharama kubwa za ufuatiliaji. Zamani ilibidi uzunguke nchi nzima kukusanya takwimu, lakini kwa sasa maisha yamekuwa rahisi zaidi maana kila kitu unapata moja kwa moja kutoka kwenye mfumo," amefafanua Bw. Valence Karunde, Mhasibu Mkuu wa TCDC.

Aidha, Bw. Karunde ameongeza kuwa matumizi ya TEHAMA kupitia mfumo wa MUVU yamechangia kwa kiwango kikubwa ongezeko la mapato ya vyama vya ushirika. Takwimu zinaonesha kuwa mapato yameongezeka kutoka Shilingi Bilioni 3.2 Mwaka 2022/2023 hadi kufikia Shilingi Bilioni 7.3 Mwaka 2024/2025, sawa na ongezeko la zaidi ya asilimia 100. Hili ni uthibitisho kuwa usimamizi wa kisasa una mchango mkubwa katika ukuaji wa sekta ya ushirika.

Kuongezeka kwa Uwazi na Uwajibikaji

Kwa mujibu wa Mkuu wa TEHAMA - TCDC Bw. Hermes Sotter, anasema kupitia Mfumo wa MUVU uwajibikaji miongoni mwa watendaji umeongezeka kwa kiasi kikubwa, kwa kuwa mfumo wa MUVU umetatua changamoto za ucheleweshaji wa maombi mbalimbali katika utendaji wa kila siku wa vyama vya ushirika.

"Kwa sasa hata kama umechelewesha malipo au maombi, yote yanaonekana kwenye mzunguko, kama ombi likikwama linaonekana limekwama kwa nani hivyo inakuwa rahisi kufuatilia kwa yule afisa ambaye hajawajibika na faili limekwama kwake," amebainisha Bw. Sotter.

Bw. Sotter ameongeza kwamba, taarifa zote muhimu kuanzia mapato, matumizi hadi gawio la wanachama zinahifadhiwa kwa njia ya kidijitali. Hatua hii imepunguza mianya ya ubadhirifu na imeongeza imani ya wanachama.Kupitia mfumo wa MUVU, kila mwanachama anaweza kuona mwenendo wa chama chake cha Ushirika, bila kusubiri vikao ambavyo aghalabu hufanyika kila robo ya mwaka.

Utekelezaji wa mfumo wa MUVU umeleta mapinduzi makubwa katika uendeshaji wa vyama vya ushirika nchini. Kupitia mfumo huu, vyama vimeweza kubainika kwa usahihi, taarifa zimehifadhiwa kwa usalama, na usimamizi wa rasilimali umekuwa wa uwazi na wa kisasa.

Hakika, MUVU si tu mfumo wa taarifa, bali ni jukwaa la mageuzi ya kweli katika sekta ya ushirika. Mageuzi haya yanapaswa kuendelezwa, kuimarishwa na kuungwa mkono na wadau wote ili kujenga ushirika wa kisasa, unaoaminika, na wenye mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa wanachama na taifa kwa ujumla.



Mhe. Athumani Kilundumya
**Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo**

# Ushirikiano wa e-GA na Sekta ya Kilimo wazidi kuimarika.

Na. Queenter Mawinda | Afisa Habari Mwandamizi

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Mhe. Athumani Kilundumya, ameipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kuimarisha ushirikiano na Sekta ya kilimo katika kuleta mapinduzi ya kidijitali katika Sekta hiyo.

Mhe. Kilundumya ameyasema hayo Agosti 4 Mwaka huu wakati alipotembelea banda la e-GA katika maonesho ya Kilimo na Wafugaji "Nanenane" yanayofanyika kitaifa katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma.

Alibainisha kuwa, Wizara ya Kilimo imeshuhudia jitihada mbalimbali zinazofanywa na e-GA katika ujenzi wa mifumo ya TEHAMA kwa kushirikiana na taasisi zilizo chini ya sekta ya kilimo ili kuimarisha sekta hiyo.

"Natambua jitihada za e-GA ikiwemo ujenzi wa Mfumo wa Usimamizi wa mbolea kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA) ambao unawezesha usajili na utoaji wa leseni kwa wauzaji na wasambazaji wa mbolea, utambuzi wa maghala ya utunzaji wa mbolea pamoja na udhibiti wa soko la mbolea" alifafanua.

Aliongeza kuwa, kupitia mfumo huo Serikali inaweza kudhibiti soko la mbolea na kuhakikisha mbolea inauzwa kwa bei rafiki kutokana na ruzuku ya Serikali katika mbolea na hivyo wakulima kuweza kulima na kupata faida.


Aidha, alitaja taasisi nyingine zilizoshirikiana na e-GA katika ujenzi wa mifumo ya TEHAMA kuwa ni pamoja na Tume ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika kwa kujenga Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushiriki na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kujenga Mfumo wa Usimamizi wa Shughuli za Umwagiliaji.

"Nafahamu kuna Mfumo wa eKilimo, ambao unarahisisha utendaji kazi katika sekta ya kilimo natamani kuona baadae mfumo huu ukituwezesha kupata taarifa za wakulima wote hata wale wadogo waliopo vijijini, ambao hawajasajiliwa. Ni imani yangu Wizara tukileta mahitaji haya e-GA mtayafanyia kazi", alifafanua.

Naye Meneja wa Mawasiliano wa e-GA, Bi. Subira Kaswaga, amemshukuru Naibu Katibu Mkuu kwa kutembelea banda la e-GA na kuahidi kufanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa sambamba na kuendeleza ushirikiano wa e-GA na sekta ya kilimo katika kuimarisha TEHAMA katika taasisi hiyo.

Alisema kuwa, e-GA imekuwa mstari wa mbele katika kutengeneza bunifu za mifumo ya kimkakati kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya kilimo ili kuleta mapinduzi ya kidijitali kwa jamii ya mijini na vijijini.

Maonesho ya kitaifa ya nanenane, Mwaka 2025 yalifanyika katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma yanaongozwa na Kaulimbiu isemayo: 'Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi'.




# Tovuti yatajwa kuwa nyenzo muhimu ya Taarifa za Serikali

Bw. Ricco Boma

Na. Queenter Mawinda | Afisa Habari Mwandamizi

Wakuu wa Vitengo vya Mawasiliano Serikalini, wametakiwa kuhuisha taarifa katika tovuti za taasisi kwa wakati, ili kuhakikisha wananchi na wadau mbalimbali wanapata taarifa sahihi za miradi ya maendeleo inayotekelezwa na huduma zinazotolewa na taasisi kupitia tovuti hizo.

Rai hiyo imetolewa na Mkurugenzi wa Huduma za TEHAMA wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) **Bw. Ricco Boma**, wakati akifungua mafunzo ya siku tatu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Tovuti za Serikali, kwa Wakuu wa Vitengo vya Mawasiliano Serikalini wa Wizara, kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi Benedict Ndomba. Mafunzo hayo yalifanyika Septemba 10 hadi 12, mwaka huu Mkoani Morogoro.

Alisema kuwa, kwa kuwa tovuti ni nyenzo muhimu ya utoaji wa taarifa rasmi za Serikali, ni muhimu kwa viongozi hao kuzisimamia vema, na kuhakikisha wanahuisha taarifa za tovuti mara kwa mara, ili wananchi waweze kufahamu mambo muhimu yanayojiri katika taasisi husika, ikiwemo utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

"Wakuu wa Vitengo vya Mawasiliano mnao wajibu wa kusimamia tovuti za taasisi zenu kwa kuzingatia misingi na kanuni za taaluma ya habari katika utoaji wa taarifa kupitia tovuti, pamoja na kufanya maboresho ya tovuti hizo pale inapohitajika ili kwenda sambamba na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia", alifafanua Bw. Ricco.

Alisema kuwa, e-GA imepewa jukumu la kusimamia tovuti za Serikali kwa upande wa kiufundi na kuwa ipo tayari kutoa msaada wakati wowote pale inapohitajika, na kuwataka Wakuu wa Idara na Vitengo vya Habari Serikalini, kutekeleza jukumu lao la kuhuisha taarifa katika tovuti zao.

Aliongeza kuwa, ili kuwa na utaratibu wa uanzishaji wa tovuti za Serikali, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, iliandaa miongozo mbalimbali, ikiwemo Mwongozo wa Matumizi bora, Sahihi na Salama wa Vifaa, Data na Mifumo ya TEHAMA Serikalini wa Mwaka 2022, pamoja na Mwongozo wa Kusimamia na Kuendesha Tovuti za Serikali wa mwaka 2014.

Katika mafunzo hayo, mada mbalimbali zikiwemo Sheria ya Serikali Mtandao, Matumizi ya Teknolojia mbalimbali katika kada ya mawasiliano Serikalini, pamoja na usalama wa tovuti na mitandao ya kijamii inayotumiwa na Serikali zilitolewa, ili kuwawezesha viongozi hao kuweza kukabiliana na changamoto za kimtandao pindi zinapojitokeza.

Naye Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano Ofisi Rais- Mipango na Uwekezaji Ndugu Raymond Mtani, ameishukuru e-GA kwa kuandaa mafunzo hayo ambayo amesema yatawajengea uwezo na kuwapa misingi bora ya usimamizi na uendeshaji wa tovuti unaofuata viwango na ubora unaohitajika.

Hadi sasa, e-GA kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za umma imefanikiwa kutengeneza zaidi ya tovuti **500**, na hivyo kuwezesha wananchi kupata taarifa za miradi ya maendeleo na shughuli mbalimbali inazozifanya kwa wakati.




# Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA yameimarisha Uwazi Na Ufanisi Serikalini

Na. Benchine Bago | Afisa Habari



Bw. Sylvan Shayo

Mkurugenzi wa Udhibiti na Usalama wa TEHAMA Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bw. Sylvan Shayo, amesema matumizi ya mifumo ya TEHAMA Serikalini yamongeza uwazi, ufanisi na kuiwezesha Serikali kuwa na uwezo mkubwa wa kuhifadhi nyaraka, na kupata kumbukumbu kwa usahihi na kwa wakati.

Bw. Shayo ameyasema hayo Agosti 26, Mwaka jijini Dar es Salaam, wakati akiwasilisha mada kuhusu matumizi ya Ofisi Mtandao ndani ya sekta za Umma, katika Kikao cha 13 cha Wataalam wa Kumbukumbu na Nyaraka, kilichoandaliwa na Chama cha Menejimenti ya Kumbukumbu na Nyaraka Tanzania (TRAMPA).

Alisema kuwa, mapinduzi hayo yamechangiwa na uwepo wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo bora ya Serikali Mtandao.

“Leo taasisi zaidi ya 380 zinatumia mifumo ya kielektroniki kuhifadhi kumbukumbu na kuwezesha utoaji wa huduma kwa haraka na kuondoa urasimu, lakini pia kwa sasa faili haziwezi kupotea wala kughushiwa kirahisi kwa sababu, taarifa zinapatikana moja kwa moja kutoka kwenye vyanzo rasmi”, alifafanua Shayo.

Aliongeza kuwa, TEHAMA imewezesha taarifa muhimu kuhifadhiwa na kufikiwa kwa urahisi bila kuhitaji mtu kuzibeba au kuzisafirisha kutoka sehemu moja hadi nyingine. Aidha Kumbukumbu na Nyaraka muhimu sasa zinapatikana kidijitali, hali inayopunguza kwa kiasi kikubwa hatari ya kughushi au kupotea kwa majalada ya Serikali.

Shayo alisema, huduma za serikali mtandao zimeboresha utendaji kazi katika sekta mbalimbali zikiwemo sekta za ardhi, elimu na afya kuanzia uombaji na utoaji wa hati miliki za ardhi, matokeo ya mitihani hadi taarifa za wagonjwa.

“TEHAMA inatulazimu kuongeza uwajibikaji, kasi na uwazi wa kweli katika utoaji wa huduma kwa umma”, alisisitiza Bw. Shayo.

Mkutano huo uliongozwa na kauli mbiu isemayo **“Matumizi ya Ofisi Mtandao ni Chachu ya kufikia Malengo Makuu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 – 2050”** uliwakutanisha Maafisa Kumbukumbu zaidi ya 1000 kutoka katika taasisi mbalimbali za Umma.



# Programu ya Mafunzo kwa Vitendo 2025 yazinduliwa Dodoma.

Na. Benchine Bago | Afisa Habari

Programu ya Mafunzo kwa Vitendo yanayoratibiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kupitia Kituo chake cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao kwa Mwaka 2025 yamezinduliwa rasmi jijini Dodoma.

Programu hiyo ya Wiki 10 hutolewa kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu wanaosomea fani ya TEHAMA, ambapo jumla ya wanafunzi 57 wanaosoma fani hiyo kutoka katika Vyuo 14 wameshiriki katika programu hiyo.

Akizungumza katika ufunguzi wa programu hiyo Agosti 02 Mwaka huu , Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi Benedict Ndomba amebainisha kwamba, lengo kuu la mafunzo hayo ni kuhakikisha wanafunzi wa Vyuo Vikuu wanapata uzoefu na picha pana ya uwiano kati ya kile wanachosoma darasani na uhalisia katika sehemu za kazi.

“Katika mafunzo haya tunahakikisha tunawapa uzoefu na kuweza kubaini juu ya uhusiano uliopo kati ya elimu ya darasani, na soko la dunia ili kuandaa taifa la leo na kesho linaloweza kushindana katika uchumi wa kidigiti”, alifafanua Ndomba.

Kwa upande wake Meneja wa Sheria wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi (SACP) Rafael Rutaihwa, amewasihi wanafunzi hao kuishi katika misingi ya uadilifu, weledi na kuheshimiana wakati wote wakiwa kituoni hapo.

Alifafanua kuwa, uadilifu na weledi hutengeneza mazingira rafiki ya ubunifu na tafiti zenye tija kwa taifa na hatimaye kuleta majibu kwa changamoto mbalimbali zilizopo kwenye jamii kupitia TEHAMA.

“Uadilifu na weledi vinahitajika kwa pamoja, kwa kuwa mmetoka katika mazingira ya vyuo mbalimbali hivyo kuheshimiana ni jambo muhimu pia, ili muweze kufanya kazi pamoja na kuelewana kwani, kipaji pekee hakiwezi kukupa matokeo chanya kama hautoweza kuishi kwenye misingi hiyo mikuu”, alisisitiza SACP Rutaihwa.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Bi. Starah Kavira, aliwataka wanafunzi hao kujikita katika kubuni mifumo itakayotatua changamoto kulingana na mazingira ya Watanzania.

Kwa upande wao wanafunzi waliojiunga na programu hiyo wameridhishwa na uwazi pamoja na mfumo uliotumika kutoa nafasi kwa vijana wa vyuo mbalimbali nchini, na kuishukuru Serikali kupitia e-GA kwa kuanzisha programu hiyo.

Wakizungumza baada ya ufunguzi, Amina Kalonge mwanafunzi wa mwaka wa kwanza kutoka chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) na Leticia Omary kutoka Chuo cha Sayansi Mbeya (MUST) wameshauri wanafunzi hasa wasichana kuomba nafasi



*Wanafunzi wanaoshiriki Mafunzo kwa Vitendo (Practical Training) wakisikiliza kwa makini mada zilizotolewa wakati wa uzinduzi wa mafunzo hayo jijini Dodoma*

hizo zinapotangazwa, ili kupata jukwaa la kuwajengea ujuzi na uzoefu katika sekta ya TEHAMA.

Katika mafunzo ya mwaka huu, e-GA imeweka maeneo ya kipaumbele ili kuwawezesha wanafunzi kujikita katika bunifu na tafiti zinazohusu teknolojia za '**Internet of Things - IoT, 'Blockchain', Cryptocurrency, Machine Learning, Akili Unde (Artificial Intelligence - AI) na teknolojia ya Usalama wa mifumo ya mtandao.**

**"Lengo la Mafunzo haya ni kuwapa ujuzi na kuongeza uwezo wa kujenga mifumo kulingana na mazingira yetu ya kitanzania, hivyo mtumie muda wenu vizuri ili kuleta ufumbuzi wa changamoto zetu".**



**Bi. Starah Kavira,**
Kaimu Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshaji.



*Viongozi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), wakiwa katika picha ya pamoja na na wanafunzi wanaoshiriki Mafunzo kwa vitendo 2025.*

# Tembea Kijididijitali:

## Mageuzi ya Huduma za Umma Kupitia e-Tour




*Afisa TEHAMA wa e-GA Bw. Claud Charles, akieleza namna Teknolojia ya Uhalisia Pepe (Virtual Reality Tour) inavyofanya kazi.*

Na. Benchine Bago | Afisa Habari

**Vipi kama mwananchi angeweza kutembelea ofisi ya Serikali, kuchunguza huduma zinazopatikana, au hata kuangalia maendeleo ya miradi ya kitaifa, yote haya bila kuinuka kutoka kwenye kiti chake nyumbani?**

Vipi kama kwa kutumia simu ya mkononi au kompyuta, mtu angeweza 'kutembea' katika miundombinu ya barabara iliyojengwa na TARURA huko Lushoto, Tanga, au kuchunguza kwa undani maendeleo ya miradi ya mafuta na gesi ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania **(TPDC)** huko Mtwara?

Hili halibaki kuwa ndoto tena. Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Maendeleo ya Serikali Mtandao cha Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kwa sasa kimebuni teknolojia ya e-Tour, licha ya kuwa kwa sasa mfumo huu upo katika hatua za awali za ujenzi, lakini ni ishara ya namna Tanzania inavyopiga hatua mpya kuelekea Serikali Mtandao yenye ufanisi, uwazi, na ujumuishi zaidi.

Mfumo huu wa kijidijitali unatoa fursa kwa wananchi kuzunguka kimtandao maeneo mbalimbali ya umma, kushiriki katika ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo, kufahamu maeneo ya urithi wa kitaifa, na hata kupata elimu kuhusu njia za tahadhari wakati wa maafa yote kwa njia ya simu au vifaa vingine vya kidijitali.

e-Tour ni zaidi ya zana ya teknolojia; ni daraja kati ya serikali na wananchi, njia ya kuongeza uwazi, uwajibikaji, na ushirikishwaji. Katika bara linalokumbwa na changamoto za miundombinu ya upatikanaji wa taarifa, Tanzania inajitokeza kama mfano wa kuigwa kwa kutumia ubunifu huu kuimarisha utoaji wa huduma za umma. Huu ndio

mustakabali wa ushirikiano kati ya raia na serikali na safari hii inaanza sasa kupitia Kituo hiki cha Utafiti na Uendelezaji wa Serikali Mtandao.

## e-Tour ni nini?

e-Tour inamaanisha Ziara ya Kielektroni kwa Teknolojia ya Uhalisia Pepe (Virtual Reality Tour). Inatumia picha na video za nyuzi 360, na wakati mwingine modeli za 3D, kuunda uzoefu wa kutazama moja kwa moja kupitia kifaa maalumu na mtazamaji kuona picha halisi kama ilivyo eneo la tukio.

Kwakutumiasimuaukompyuta, wananchi wataweza kutembea hospitalini, kukagua mradi wa barabara, au hata kuangalia kituo cha huduma kabla hawajafika. Kwa serikali, hii si tu ni njia ya kisasa ya kuonyesha miradi pekee, pia ni nyenzo ya kuongeza uwazi, kuboresha huduma, kurahisisha ufuatiliaji na kupunguza gharama.

Zana ya Uwajibikaji na Uwazi
Moja ya hoja kuu za kutumia EVR-Tour katika utawala ni uwazi. Katika nchi nyingi za Afrika, imani ya wananchi kwenye miradi ya serikali mara nyingi hupungua kutokana na ukosefu wa ufuatiliaji wa wazi.

Wananchi husikia kuhusu daraja jipya, hospitali au barabara, lakini ni wachache wanaoweza kuona maendeleo kwa macho yao, kulingana na umbali wa eneo ambalo mradi umetekelezwa na wao walipo. Kupitia ziara za mtandaoni kwa mfumo wa e-Tour, serikali itaweza kuruhusu wananchi hata wa vijijini au walio nje ya nchi kushuhudia hatua halisi ya mradi hiyo.

Fikiria mradi wa barabara unaotekelezwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) au Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ambapo wananchi wanaweza kubofya na kulinganisha picha za nyuzi 360 kila mwezi, kuanzia wakati wa kuanzishwa hadi kukamilika.

Aidha, taasisi za umma inaweza kutumia ziara za e-Tour kwa mafunzo ya wafanyakazi badala ya kuwasafirisha wengi kwenda eneo la mradi.

## Kurahisisha Huduma kwa Wananchi

Kwa Mtanzania wa kawaida, e-Tour inaweza kubadilisha kabisa jinsi ya kufikia huduma za serikali. Ziara ya mtandaoni inaweza kuwa kama mwongozo wa kidijitali, ikionyesha dirisha sahihi, nyaraka zinazohitajika, na hatua za kufuata kabla ya kufika.

Kwa mfano, Hospitali ya Taifa Muhimbili au Benjamin Mkapa inaweza kuwa na ziara ya dakika mbili inayoelekeza mgonjwa moja kwa moja kwenye kliniki husika, ikionyesha sehemu za malipo na nyaraka zinazohitajika.

Matokeo yake ya e-Tour ni kupunguza misongamano, huduma bora zaidi, na kuridhika kwa wananchi kuhusu utoaji wa huduma katika taasisi za Umma.

## Mipango na Ushirikishwaji

Maendeleo ya miji ni eneo jingine lenye fursa kubwa ya matumizi ya e-Tour. Kwa mfano jiji la Dodoma linapanuka kwa kasi na miradi mipya ya masoko au vituo vya mabasi inahitaji maoni ya wananchi. Badala ya ramani za kawaida, wapangaji wanaweza kuchapisha picha za nyuzi 360 za maeneo yaliyopendekezwa. Wananchi wanaweza kutembelea miradi hiyo ya maendeleo, kutoa maoni, au kuuliza maswali kabla ya ujenzi kuanza.

Hii ni njia ya mipango shirikishi, inayowezesha jamii kushiriki maamuzi. Pia, inahakikisha usawa kwani makundi maalum kama watu wenye ulemavu wanaweza kutembelea eneo hilo mtandaoni na kujua iwapo jengo lina njia za kupanda au vyoo rafiki.

## Utalii na Urithi wa Utamaduni

Utalii ni nguzo muhimu ya uchumi wa Tanzania, na e-Tour inaweza kuwa chombo cha kipekee cha kuutangaza. Ziara za mtandaoni za Hifadhi ya Serengeti, Bonde la Ngorongoro, au miji ya kihistoria kama Bagamoyo na Kilwa Kisiwani zinaweza kuwashawishi watalii wa kimataifa kuja nchini kwa kuonesha kipande kifupi cha nyuzi 360 kupitia e-Tour.

## Mafunzo, Usalama na Maafa

Taasisi za serikali zinazohusika na usalama pia zinaweza kufaidika. Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) au Ofisi ya Waziri Mkuu inayosimamia maafa zinaweza kutumia e-Tour kuonyesha maeneo hatarishi kwa mafuriko, kuelekeza njia za kuokoa maisha, au kuonyesha makazi salama wakati wa majanga. Katika nyakati za dharura, wananchi wanaweza kufikia maelekezo haya kwa urahisi kupitia simu janja zao.

e-Tour inasadifu vyema malengo haya, ikitoa suluhisho rahisi na lenye matokeo ya moja kwa moja. Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao kinaendelea na utafiti na ubunifu wa mfumo huu, ili kuhakikisha unafikia hatua za majaribio na hatimaye kuweza kutumika kabisa.



# Mgongo Wako, Afya Yako: Tambua Hatari, Epuka Maumivu

**Jifunze mbinu bora za kujikinga na matatizo ya mgongo kwa kubadili mtindo wa maisha.**

Na Queenter Mawinda | Afisa Habari Mwandamizi

Maumivu ya mgongo ni moja ya tatizo la kiafya linalowaathiri watu wa rika na jinsia zote, na mara nyingi husababishwa na mchanganyiko wa sababu nyingi kutokana na eneo lililoathirika. Sababu hizi zinaweza kuwa za kimwili, kiafya na hata mitindo ya maisha.

Watu wengi hupata maumivu haya kwa nyakati tofauti katika maisha yao. maumivu haya yanaweza kuathiri sana maisha ya kila siku na uwezo wa kufanya kazi au majukumu ya familia. Daktari Bingwa wa Mifupa kutoka Hospitali ya Benjamini Mkapa Kitengo cha Mifupa, Ubongo na Mishipa ya fahamu jijini Dodoma Dkt. Mugisha Nkoronko, anatuhabarisha kuwa matatizo haya ya maumivu ya mgongo huwapata zaidi wanawake kwa asilimia 60-65, wakifuatiwa na wazee ambao huathirika na uchakavu wa mifupa kutokana na umri wao, na kufuatiwa na watoto kuanzia miaka 5-8 kutokana na michezo, majeraha au kulala vibaya.

Katika Makala hii Dkt. Nkoronko atatuhabarisha kuhusu chanzo, dalili, kinga na matibabu ya maumivu ya mgongo.

## Chanzo cha maumivu katika uti wa mgongo

- Kukaa au kulala kwa mikao isiyofaa, hasa kwenye viti visivyokidhi viwango vya kiafya, kunaweza kusababisha maumivu ya mgongo
- Kubeba au kuinua vitu vizito kichwani bila kuchukua tahadhari husababisha mkazo mkubwa kwenye mgongo na kuongeza hatari ya majeraha.
- Kunyanyua vitu vizito bila kutumia mkao sahihi huweza kusababisha madhara katika misuli na pingili za mgongo
- Ajali au majeraha yanayotokea wakati wa michezo huweza kuathiri misuli, mishipa na pingili za mgongo, na hivyo kusababisha maumivu ya kudumu
- Kutokulala sehemu nzuri kama vile kutumia godoro ambalo halitoi msaada wa mgongo huongeza hatari ya kupata maumivu ya mgongo.
- Uzito kupita kiasi
- Kubeba watoto mgongoni na kufanya shughuli za nyumbani zinazohusisha kuinama mara kwa mara husababisha mkazo wa mara kwa mara kwenye mgongo, na hivyo kuongeza uwezekano wa kupata maumivu ya mgongo.

## Dalili za Magonjwa ya Uti wa Mgongo

Dalili za magonjwa ya uti wa mgongo zinaweza kutofautiana kulingana na aina ya ugonjwa, kiwango cha uharibifu na sehemu ya uti wa mgongo iliyoathirika. Watu wengi huchanganya maumivu ya mgongo bila kuwa na uhakika wa eneo halisi lililoathirika.

Hapa Dkt. Nkoronko anatueleza dalili kuu zinazoweza kuashiria matatizo ya uti wa mgongo kuwa ni pamoja na;-

- kupata maumivu yanayoweza kusababishwa na athari kwenye misuli, mifupa, neva au diski ya uti wa mgongo.
- Kupata ganzi miguuni na mikononi
- Kupoteza fahamu (kushindwa kutembea, mkojo kutoka wenyewe).
- Ikiwa dalili hizi zitajitokeza, ni muhimu sana kushauriana na daktari kwa uchunguzi wa kina ili kupata tiba sahihi.
- Waswahili husema Kinga ni bora kuliko Tiba. Dkt. Nkoronko anatuhabarisha baadhi ya tahadhari za kuchukua ili kuepukana na matatizoyanayoweza kuambatana na maumivu ya mgongo;-
- Kuepuka shughuli zinazoweza kusababisha mkazo kwenye mgongo

Asilimia kubwa ya kina mama ni walezi wa familia. Hivyo majukumu mengi ya nyumbani hutekelezwa na wanawake. Wanawake hujikuta wahanga wa matatizo ya uti wa mgongo, kwani wamekuwa wakifanya shughuli nyingi za nyumbani ambazo zinahusisha kuinama mara kwa mara na kupelekea madhara kwenye mgongo.

Pia, ubebaji wa watoto mgongoni hupelekea athari ya kiwango kikubwa kwenye mgongo. Dkt. Nkoronko anawashauri wakina mama, kuepuka shughuli zinazopelekea kuinama au kubeba vitu vizito mgongoni kama vile, kubeba mtoto muda mrefu, kwani husababisha mkazo kwenye misuli na mishipa ya mgongo na hatimaye kuleta athari kwenye diski ya uti wa mgongo.

- **Kuepuka kukaa muda mrefu kwenye kiti**

**"Ni vema kwa wafanyakazi wa ofisini, kutumia viti vinavyokidhi viwango vya kiafya wakati wa kutekeleza majukumu yao ya kiofisi, lakini pia wanapaswa kuepuka kukaa mkao mmoja kwa muda mrefu", Dkt. Nkoronko.**

Ukaaji wa mkao mmoja kwa muda mrefu huweza kuleta athari katika diski ya uti wa mgongo. Hivyo, kila baada ya masaa mawili, inashauriwa kunyanyuka na kufanya mazoezi ya kutembea tembea.

Tahadhari hii inatolewa pia kwa madereva, hasa wa masafa marefu kwani wanatumia muda mwingi kukaa na kuendesha gari. Madereva wanashauriwa kutumia mto utakaosaidia shingo kuwa katika mstari mmoja na mgongo na hivyo kutoa msaada mzuri wa mgongo wakiwa safarini.

- **Usingizi ni Tiba**.

"Ingawa mara nyingi hatuufikirii usingizi kama sehemu ya matibabu ya mgongo, usingizi mzuri unaweza kusaidia kupunguza maumivu, kuimarisha misuli, na hata kuzuia matatizo ya mgongo", anafafanua Dkt. Nkoronko.

Dkt. Nkoronko anasisitiza umuhimu wa kulala kwenye godoro zuri ili kuipa misuli ya mgongo nafasi ya kupumzika na kujirekebisha baada ya shughuli za siku. Hali hii hupunguza mkazo na maumivu ya misuli.

- **Kubadili Mtindo wa Maisha**

Mtindo wa maisha una mchango mkubwa katika afya ya mgongo aidha kwa kuimarisha au kuharibu. Maamuzi tunayofanya kila siku kuhusu lishe, mazoezi na mikao, yote yanaweza kuathiri mgongo kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja.

Dkt. Nkoronko anashauri kuzingatia afya kwa kufanya mazoezi mara kwa mara ili kuimarisha misuli ya msingi, ambayo ni nguzo ya afya ya mgongo. Aidha, uzito kupita kiasi hasa kwenye tumbo huongeza mzigo kwa mgongo wa chini na kusababisha maumivu ya mara kwa mara.

- **Kuzingatia Sheria za Usalama Barabarani**

Kwa madereva wa vyombo vya moto, ni vyema kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuepukana na ajali ambazo zinaweza kuzuilika. Dkt. Nkoronko anasema, ajali zinaweza kusababisha diski ya mgongo kushtuka au kutoka mahali pake 'slipped disc'. Hali hii husababisha maumivu makali, na mara nyingine ganzi. Umakini kwenye michezo pia, ni jambo la msingi kwani majeraha ya michezo huweza kuharibu misuli, diski za uti wa mgongo au neva za mgongo.

## Tiba mbalimbali za mgongo

**Tiba ya kwanza.** Mgonjwa kufanya mazoezi maalum ya mgongo (Fiziotherapia), ambayo hutolewa hospitalini kwa watu wenye tatizo la mgongo kupinda, kwa sababu ya kukaa vibaya au pingili nyingi kuvimba, ambazo haziwezi kupata matibabu ya njia nyingine.

**Tiba ya pili.**
Kutumia dawa zinazolainisha misuli na kurejesha afya kwenye mishipa ya fahamu. Hata hivyo, hakuna dawa zinazorejesha diski za uti

wa mgongo zilizovimba au zilizopasuka.

Ingawa Dkt. Nkoronko anasema tatizo linapokuwa kubwa sana basi hufanyiwa Tiba ya tatu, ambayo ni upasuaji maalum. Tiba za upasuaji hurekebisha mifupa na diski zilizoharibika, ambapo kuna vigezo ambavyo mtu inabidi avifikie ili kufanyiwa upasuaji huo.

**Tiba ya nne** na ya mwisho inahusisha matibabu yote kwa pamoja yani mazoezi, dawa na upasuaji.
Afya ndio mtaji namba moja. Dkt. Nkoronko anasema maumivu ya mgongo yanaweza kuwa kero kubwa, lakini kwa kujua sababu, dalili na namna ya kujikinga, mtu anaweza kuepuka au kuyadhibiti kwa ufanisi.

Anatoa wito kwa jamii yote, kuzingatia mtindo wa maisha kwa kufanya mazoezi na kupunguza uzito ili kuepukana na athari zinazoweza kujitokeza katika mgongo.

Pia ameshauri kuzingatia lishe kwa kula vyakula visivyokobolewa na vyakula vinavyoupa mfumo wa fahamu afya kama vile, mbogamboga, vyakula vyenye madini ya 'calcium' kama vile Samaki, maziwa, vyakula vya jamii ya mbegumbegu kama korosho, karanga na mwani.

Pale maumivu yanapoendelea kwa muda mrefu na kuwa makali, Dkt. Nkoronko anashauri ni muhimu kutafuta msaada wa kitabibu. Kujali mgongo wako ni sehemu muhimu ya kujali afya yako kwa ujumla.



*Daktari Bingwa wa Mifupa kutoka Hospitali ya Benjamini Mkapa Kitengo cha Mifupa, Ubongo na Mishipa ya fahamu Dkt. Mugisha Nkoronko, akitoa Elimu ya magonjwa ya Mifupa kwa Afisa Habari Mwandamizi wa e-GA Bi. Queenter Mawinda wakati alipofanya mahojiano kuhusu magonjwa ya Mifupa.*

# Mafunzo kwa Vitendo

Wanafunzi wa Vyuo Vikuu katika fani ya TEHAMA walioshiriki program ya Mafunzo kwa Vitendo Mwaka 2025, katika Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao cha e-GA, wametoa maoni kuhusu program hiyo;




"Kwa upande wangu, mimi ni mwanafunzi wa mwaka wa kwanza, na kupitia programu hii nimepata uzoefu mzuri sana. Sasa ninajua kwamba nikifika mwaka wa pili, nitakuwa na uelewa mpana zaidi wa kile ninachojifunza kwa sababu nimekwishajifunza mambo hayo katika mazingira halisi ya kazi — iwe ni maofisini au viwandani."

**LETICIA ARTHUR OMARI**
Mwanafunzi Chuo Kikuu cha Sayansi Mbeya (MUST)



"Tulipoanza, nilifikiri nitajifunza kutengeneza tovuti au programu za simu pekee, lakini baada ya kuanza rasmi, tuliweza kuchunguza maeneo mengi zaidi. Tulijifunza kuhusu Cyber Security, Internet of Things (IoT), na Blockchain. Haya yote yamenisaidia sana kupanua upeo wa maarifa yangu ya kiteknolojia na kunisaidia kufanya maamuzi sahihi kuhusu taaluma yangu ya baadaye."

**KELVIN BABYATO ARTHUR OMARI**
Mwanafunzi Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam (UDSM)



"Miongoni mwa faida kubwa nilizopata kupitia programu hii ni kujifunza kufanya kazi katika mazingira halisi (real-world situations). Chuoni, tunafundishwa zaidi kwa nadharia, na mara nyingi kazi za vitendo huwa zinatumia mazingira ya kufikirika. Lakini hapa, tumepata fursa ya kufanya kazi halisi na kuongeza ujuzi wa vitendo zaidi."

**MESHACK CHANAI**
Mwanafunzi Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)



"Programu ya Mafunzo kwa Vitendo ni programu maalum iliyoandaliwa kwa ajili ya wanafunzi wa vyuo ili kuwasaidia kupata uelewa na ujuzi wa vitendo, tofauti na ule wa nadharia wanaoupata darasani. Hapa, wanafunzi hupata nafasi ya kufanya mafunzo kwa vitendo zaidi na kuelewa uhalisia wa kazi tofauti na wanavyofikiri wakiwa vyuoni."

**GILLIAN MBOYA**
Mwanafunzi Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)

# Maonesho




*Afisa Habari Mwandamizi wa e-GA Bi. Catherine Peter, akitoa Elimu kwa mwananchi aliyetembelea banda la maonesho la Mamlaka ya Serikali Mtandao wakati wa maonesho ya Sabasaba yaliyofanyika jijini Dar Es Salaam.*




*Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Dkt. Jabir Bakari, akipokea maelezo kutoka kwa Afisa Habari Mwandamizi wa e-GA Bi Queenter Mawinda, wakati alipotembelea banda la e-GA katika maonesho ya Nanenane Jijini Dodoma.*

# Kikao cha Bodi ya Wakurugenzi ya e-GA



*Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao Dkt. Mussa Kissaka, akiongoza kikao cha Bodi kilichofanyika Septemba 2025 katika Ofisi za Mamlaka zilizopo Mjini Iringa.*



*Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya mamlaka ya Serikali Mtandao Dkt. Mussa Kissaka (katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na wajumbe wa Bodi na Menejimenti ya Mamlaka ya Serikali Mtandao mara baada ya kumaliza kikao cha Bodi Mjini Iringa.*

# BODI YA KWANZA YA WAKURUGENZI YA MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO



***Dr. Mussa Kissaka***
***Chairperson***



Dr. Jasmine Tiisekwa
*Vice Chairperson*



Justina Mashiba
*Member*



Angelista Kihaga
*Member*



Prof. Aloys Mvuma
*Member*



Eric Shitindi
*Member*



Priscus Kiwango
*Member*



Francis Kayichile
*Member*



Dr. Lorah B Madete
*Member*

**Ofisi ya Rais,**
**Mamlaka ya Serikali Mtandao**
**Mtumba-Mtaa wa Mtandao,**
**S.L.P 2833,**
**40404 DODOMA.**
**Baruapepe: barua@ega.go.tz**
**Simu +255 026 - 296 1957**

"Karibu tuijenge Serikali Kidijitali"